



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA
ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA
UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA 14 ZA
TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha uchaguzi mdogo wa Madiwani katika kata 14 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Alhamis, tarehe 13 Julai, 2023 katika kata zifuatazo: -

| Na. | Kata | Halmashauri |
|------------|-------------|--------------------|
| 1. | Bosha | Wilaya ya Mkinga |
| 2. | Bunamhala | Mji wa Bariadi |
| 3. | Kalemawe | Wilaya ya Same |
| 4. | Kalola | Wilaya ya Uyui |
| 5. | Kinyika | Wilaya ya Makete |
| 6. | Kwashemshi | Wilaya ya Korogwe |
| 7. | Magubike | Wilaya ya Kilosa |
| 8. | Mahege | Wilaya ya Kibiti |
| 9. | Mbede | Wilaya ya Mpimbwe |
| 10. | Mnavira | Wilaya ya Masasi |
| 11. | Ngoywa | Wilaya ya Sikonge |
| 12. | Njoro | Wilaya ya Same |

| Na. | Kata | Halmashauri |
|-----|---------|-------------------|
| 13. | Potwe | Wilaya ya Muheza |
| 14. | Sindeni | Wilaya ya Handeni |

Kwa mujibu wa kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mdogo. Uchaguzi huo utafanyika katika kata 14 zilizopo katika halmashauri 13 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe: info@nec.go.tz au uchaguzi@nec.go.tz. Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 14 hadi 20 Juni, 2023.

Barua ya maombi inatakiwa kuianisha mambo yafuatayo kuhusu taasisi na asasi husika: -

- i. Iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- ii. Iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- iii. Ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;


- iv. Katika utendaji wake iwe haijahushwa na uchochezi au kuvuruga amani; na
- v. Iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, maombi hayo yanatakiwa kuambatishwa na: -

- i. Nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- ii. Nakala au kivuli cha Katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;
- iii. Majina ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia;
- iv. Anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake; na
- v. Ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha za kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Limetolewa leo tarehe 14 Juni, 2023 na,


Kailima, R. K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI